

BARAZA LA WAFANYAKAZI LA WIZARA YA KAZI NA AJIRA LAKUTANA.

Naibu Waziri wa Kazi na Ajira Mhe.Dkt.Makongoro Mahanga amesema upo umuhimu mkubwa wa kuwepo kwa Baraza la Wafanyakazi mahala pa kazi kwa lengo la kuleta ustawi na maendeleo ya Wafanyakazi na Taasisi husika.

Naibu Waziri aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akifungua Baraza la Wafanyakazi la Wizara ya Kazi na Ajira lililofanyika kwenye ukumbi wa Mwl.Nyerere tarehe 25/4/2015 na kuhudhuriwa na Wafanyakazi wa Wizara.

Katika hotuba yake Naibu Waziri alifafanua kuwa, mkutano huo upo kwa mujibu wa sheria Na 6 ya mwaka 2004 na pia kifungu na 73 cha sheria hiyo pamoja na miongozo mingine inayotolewa na Serikali ambapo kimefafanua na kuelezea umuhimu wa dhana ya ushirikishwaji wa Wafanyakazi katika sehemu zao za kazi kwa lengo la kuleta au kuongeza tija na ufanisi ili kuweza kufikia matarajio yaliyokusudiwa.

Aidha, Dkt Mahanga aliongeza kuwa,Baraza la Wafanyakazi licha ya kudumisha dhana ya ushirikishwaji pia lina jukumu la kuishauri Serikali juu ya ufanisi wa kazi na hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kuongeza uzalishaji,vilvile kushauri Serikali juu ya mambo yanayohusu maslahi ya Wafanyakazi na pia kuleta mabadiliko ya kanuni za utumishi na masharti ya kazi pamoja na kupokea,kujadili na kudhibitisha mipango na makisio ya mapato na matumizi ya Taasisi husika.

Sambamba na hilo alisema kuwa, dhana ya ushirikishwaji kwa kupitia mikutano mbalimbali ikiwemo Baraza la Wafanyakazi katika ngazi ya maamuzi inapelekea

kufikia hatua ya kuainisha namna nzuri ya kutekeleza mipango inayohusu Taasisi kwa kuweka bayana shughuli zilizokusudiwa kutekelezwa na kufikia lengo husika.

Baraza la Wafakazi lilihudhuriwa na Wafanyakazi na viongozi kutoka kwenye Idara na Vitengo wa Makao Makuu ya Wizara, Wawakilishi kutoka kwenye Taasisi zilizopo chini ya Wizara, Wafanyakazi kutoka kwenye ofisi za Wizara zilizopo mikoani ikiwemo mikoa ya Mwanza na Iringa pamoja na viongozi wa mkoa wa shirikisho la vyama vya wafanyakazi **(TUCTA)**.